# UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI WA MOFOLOJIA PAMOJA NA UMILISI WA KIWANGO CHA CHINI MIONGONI MWA WANAFUNZI WA VYUO VIKUU NCHINI UGANDA

*Mulei Martin*

**Ikisiri**

*Ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya isimu katika lugha ya Kiswahili vyuoni umeathiriwa na changamoto kadhaa. Miongoni mwazo ni matumizi ya misamiati ya kisayansi ambayo imeathiri upataji na ukuaji wa umilisi wa taaluma za kiisimu. Makala hii inalenga kufafanua dhana muhimu katika uchunguzi na uchambuzi wa mofolojia, kuonesha changamoto za ujifunzaji na ufundishaji wake, na kutoa mapendekezo ya kuondokana na changamoto hizo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu nchini Uganda na kwingineko. Data ilikusanywa kupitia kwa mijadala shirikishi na usaili kutoka kwa wanafunzi 70 na walimu 9 wa isimu walioteuliwa kimaksudi kutoka katika vyuo vikuu vitatu nchini Uganda. Matokeo yaliyoelezwa kwa muundo wa kimaelezo yalidhihirisha changamoto za kiisimu na zisizo za kiisimu zilizoathiri upataji wa umilisi wa somo la mofolojia. Nazo ni pamoja na: umilisi wa chini katika matumizi ya Kiswahili sanifu, ugumu na kukanganywa katika kueleza dhana za kimofolojia, mitazamo hasi, pamoja na uchache wa vitabu vya isimu vinavyokidhi masilahi ya wanafunzi wa viwango vyote vya umilisi. Utafiti ulipendekeza kuwapo kwa mijadala na makongamano, uandishi wa vitabu mwafaka vya isimu, na kujenga uchanya wa ujifunzaji wa somo la mofolojia.*

## Utangulizi

Kiswahili kinafundishwa katika vyuo vikuu kadha nchini Uganda. Takribani kila chuo kinafundisha Kiswahili kuanzia kiwango cha vyeti hadi shahada ya uzamili. Mofolojia ni somo la isimu linalofundishwa kwa lengo la kukuza umilisi wa wanafunzi wa kutambua miundo ya maneno, kuendeleza umilisi wa uandishi wa maneno, usomaji, uainishaji wa maneno na kujenga maana ya lugha inayohusika (Wainaina, Pauline, Buliba, & Gwachi, 2017). Ingawa wanafunzi wanapokea mafunzo ya somo hili, tafiti za awali zimeripoti kuwa umilisi wa somo hili ni wa kiwango cha chini sana. Jaika (2017) na Buliba (1998) wameonesha changamoto za ujifunzaji na ufundishaji wa lugha ya pili, mwingiliano wa L1 katika L2, ugumu wa upataji wa lugha ya pili kutumia umilisi wa L1, na athari za viwango vya umilisi wa fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki kama masomo ya isimu.

Makala hii inajadili matokeo ya utafiti juu ya ujifunzaji na ufundishaji wa dhana za mofolojia ambazo ni muhimu katika uchunguzi na uchambuzi wa mofolojia, kudhihirisha changamoto za ujifunzaji na ufundishaji, na mapendekezo ya kuondokana na changamoto husika ili kujenga umilisi wa mofolojia miongoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu. Hivyo, makala hii inakusudia kuchangia taluma ya isimu na kuwaongoza wahadhiri na wanafunzi kuweka mikakati ya ukuzaji na uendelezaji wa umilisi wa ufundishaji na ujifunzaji wa mofolojia na matawi mengine ya kiisimu**.**

**Historia Fupi ya Lugha ya Kiswahili Nchini Uganda**

Kiswahili kiliingia nchini Uganda mnamo mwaka wa 1844, kikafundishwa na kutumika katika mamlaka ya Kabaka Mutesa wa kwanza. Mnamo mwaka 1862, Kiswahili kilianza kuzungumzwa katika ufalme wa Bunyoro. Hii ilikuwa kabla ya kuja kwa wakoloni. Mnamo mwaka 1912, Kiswahili kilianza kufundishwa katika shule za msingi na upili. Mnamo mwaka 1927, Kiswahili kilipendekezwa kutumiwa na serikali ya kikoloni kama lugha rasmi na lugha ya kufundishwa shuleni (Mlacha, 1995).

Mwaka 1950, serikali ya kikoloni ilipendekeza Kiswahili kuwa lugha rasmi ya kitaifa licha ya kufutilia mbali ufundishaji wa Kiswahili shuleni mwaka 1941 kwa madai kuwa Kiswahili ni lugha ya Waarabu. Aidha, Kiswahili kilipendekezwa kufundishwa shuleni kwa ajili ya muungano wa wafanyakazi wa Afrika Mashariki hadi mwaka 1953. Baadaye, Kamati ya De Bansen ilipinga lugha ya Kiganda au Kiswahili kuwa lugha rasmi. Haya yote yalifanyika kutokana na upinzani uliokuwepo kati ya Wamishenari na Ufalme wa Uganda kuhusiana na lugha rasmi (Mukuthuria, 2006).

Baada ya Uganda kupata uhuru mnamo mwaka 1962, bunge la Uganda lilipitisha Kiswahili kufundishwa shuleni na kutumika kama lugha rasmi nchini Uganda. Hata hivyo, uamuzi huu haukutiliwa maanani na serikali kutokana na migogoro ya uongozi na siasa za kikabila (Mazrui, 1995).

Mnamo mwaka 1973, Idi Amini alitangaza lugha ya Kiswahili kuwa lugha rasmi ya taifa baada ya mijadala mbalimbali bungeni pamoja na upigaji wa kura ya maoni kuchagua lugha rasmi kati ya Luganda na Kiswahili. Hata baada ya Kiswahili kupitishwa kama lugha rasmi, mikakati ya utekelezaji haikuwekwa. Mnamo mwaka 1974, Kiswahili kilianza kufundishwa katika Chuo Kikuu cha Makerere. Mwaka 1979 serikali ya Idi Amini iliondolewa madarakani na wanajeshi wa Tanzania. Baada ya hapo, watu wakaanza kujifunza lugha ya Kiswahili kwa kutangamana na wanajeshi hao. Hata hivyo, vitendo vyao vilisababisha lugha ya Kiswahili kuchukiwa na kuhusishwa na mambo mengi hasi, kama vile lugha ya wakatili, wezi,

na madikteta. Licha ya kipingamizi hicho, mwaka 1986 Kiswahili kilianzishwa katika Chuo cha Ualimu Kakoba (Mlacha, 1995).

Mnamo mwaka 1992, jarida la serikali kuhusu sera za kielimu la *Government White Paper* lilipendekeza Kiswahili kufundishwa shuleni kwa madhumuni ya Kitaifa na ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kiswahili kilipitishwa na bunge kuwa lugha rasmi katika miaka ya 2005, 2006, na 2009. Hivi sasa ni somo la lazima katika shule za upili (NCDC, 2018). Aidha, mapendekezo yao yalisababisha vyuo vingi kuanzisha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kuanzia ngazi ya astashahada (cheti), stashahada na shahada. Ingawa Kiswahili kinafundishwa hivi sasa katika vyuo kadhaa nchini Uganda, umilisi wa kiisimu, hususani fonolojia, mofolojia, sintaksia, semantiki na pragmatiki, miongoni mwa wajifunzaji umeripotiwa kuwa wa viwango vya chini (Jaika, 2017 na Buliba, 1998).

## Dhana ya Mofu, Mofimu na Alomofu katika Ujifunzaji wa Mofolojia

Dhana za mofu, mofimu na alomofu ni muhimu sana katika uchambuzi na uchanganuzi wa mofolojia ya Kiswahili (Mgullu, 1999). Vilevile, Mgullu (2018) anaonesha utata wa kuelezwa kwa dhana hizi kisayansi kama ilivyoelezwa na Marealle (1978).

Wesama (2003), naye anatoa fasili ya mofolojia kuwa taaluma ya isimu ambayo huchunguza maumbo ya maneno, hususani maumbo ya mofimu. Mtazamo huu unadhihirisha dhima ya vipashio hivi vya kimofolojia. Hii ina maana kuwa mwanafunzi anastahili kuelewa mofimu na alomofu. Aidha, ili kuelewa dhana ya alomofu, mwanafunzi anastahili kuelewa dhana ya mofu kisha, kueleza kanuni zinazohusika katika utaratibu wa uundaji wa maneno.

## Dhana ya Mofolojia

Wanaisimu mbalimbali wameifasili taaluma ya Mofolojia kwa namna tofauti. *Kamusi ya Isimu na Lugha* (1990) inafasili mofolojia kama “tawi la isimu ambalo huchunguza maneno na aina za maneno”. Kihore, Massamba, na Msanjila (2003) wanaelezea kuwa mofolojia ni tawi linalochunguza vipashio vya uundaji wa maneno na taratibu zinazotumika katika uundaji wa maneno ya lugha. Kulingana na fasili hii ni muhimu kutambua vipashio husika ambavyo Kihore na wenzake wanazungumzia. Mgullu (1999) anasema kuwa mofolojia ni taaluma ya sarufi ambayo inalo jukumu la kuyachunguza maneno ili kuelewa maumbo yake yalivyo. Habwe na Karanja (2007) wanaeleza kuwa mofolojia ni neno linalotumiwa kumaanisha utanzu wa isimu unaoshughulikia muundo wa ndani wa maneno. Wanaelezea kuwa mofolojia huchunguza mofimu, aina za mofimu, namna mofimu zinavyojenga maneno, na mahusiano ya mofimu katika uundaji wa maneno.

Kwa jumla, mofolojia ni taaluma ya isimu inayoshughulika na uchunguzi na uchambuzi wa maumbo ya maneno ya aina mbalimbali katika Kiswahili. Taaluma hii huwa na jukumu la kuchunguza maneno kwa kuzingatia vipashio mbalimbali vinavyojenga au kuunda maneno, pia kuchunguza na kuchambua utaratibu wa upangaji wa vipashio husika katika kuunda maneno yenye maana. Vipashio ni vijenzi vya maumbo ya maneno ambavyo ni mofu, mofimu na alomofu. Vijenzi hivi ni muhimu sana katika ufundishaji na ujifunzaji wa tawi la mofolojia ambavyo wanafunzi hawana budi kujifunza ili kupata umilisi wake.

**Dhana ya Mofu**

Mofu ni kipashio cha kimaumbo kinachowakilisha mofimu. Mgullu (1999) anaelezea kuwa mofu ni umbo la neno ambalo huwakilisha mofimu na ambalo hudhihirika kifonolojia na kiothografia. Maelezo haya yanadhihirisha kuwa mofu ni kipashio ambacho kinaweza kutamkwa na kuandikwa kuwakilisha maana fulani katika neno. Kipashio hiki ni kikubwa kuliko fonimu na kidogo kuliko neno. Aidha, Habwe na Karanja (2004) wanaifasili mofu kama kipashio kidogo cha neno chenye maana. Maelezo yao yanalinganisha mofu na viambishi. Wanadai kuwa maumbo yoyote ambayo yanaweza kuongezwa kwenye mzizi wa neno ili kuleta maana mbalimbali za kisarufi ni vipashio vya lugha ambavyo huwakilisha dhana ya mofu. Kwa hivyo, kwao, mofu ni vipashio mbalimbali vinavyowakilisha maana ya mofimu. Maana ya mofu huweza kuwa ni ya kisarufi au kilekisika. Mofu huwa na maana ya kisarufi kutokana na kuwa maana inayojitokeza hutokana na uamilifu wa mzungumzaji wa lugha fulani. Kwa mfano:

| | |
|---|---|
| Alimpiga | {a}+{li}+{m}+{pig}+{a} |
| Atakuita | {a}+{ta}+{ku}+{i}+{ta} |

Maumbo {a}, {li}, {m} katika (a) ni mofu ya kisarufi ambayo maana yake inatokana na matumizi yake katika kishazi husika. {a} ikiwakilisha nafsi ya tatu, {li} mofu ya wakati, {m} ni kiwakilishi cha mtendwa. Hizi ni mofu ambazo huambatanishwa kuunda neno lenye maana, na zikiondolewa katika muktadha wa matumizi haziwezi kupata maana. Vilevile, mofu huweza kuwa na maana ya kilekisika kutokana na maana inayofahamika na watumiaji wa lugha fulani. Hizi ni mofu zisizoambatanishwa na mofu nyingine kuunda neno lenye maana kamili. Mifano ya mofu hizi ni: {baba}, {mama}, {shangazi}, {kaka}, na {dada}. Hii ni mofu moja yenye maana kamili. Mofu ni vipashio ambavyo haviwezi kugawanywa kwa vipashio vidogo zaidi. Vikigawanywa zaidi hivyo hupoteza maana ya kisarufi na kilekisika.

Kwa misingi ya fasili ya wanaisimu, mofu ni kipashio kidogo cha kimaumbo kinachowakilisha maana ya mofimu na hudhihirika katika matamshi na maandishi. Hii inamaanisha kuwa mofu ni sehemu ya maumbo ya maneno yenye kubeba maana ya mofimu ambayo ni ya kisarufi au ya kilekisika. Mifano katika Na. (1a) – (1e) inaonesha aina za mofu na mifano ya mofu katika kila kategoria:

(1) Mifano ya mofu

a) Mofu huru {baba}, {mimi}, {safi}, {upesi}, {tafiti}, {mbele}, {halafu}.
b) Mofu tegemezi {m}+{ti}, {ji}+{cho}, {ji}+{su}, {ku}+{fug}+{a}
c) Mofu tata {a}+{li}+{m}+{pig}+{i}+{a}
d) Mofu changamano {Mw} +{anamaji} {wa} +{anahewa}
e) Mofu kapa {Ø}+{samaki}, {Ø} +{nyumba}

**Aina za mofu**

Mofu za Kiswahili huweza kuainishwa kwa kutumia maumbo ya ndani. Katika uainishaji huu, mofu huainishwa kwa kuzingatia vigezo vikuu viwili, kigezo cha maana na kimaumbo.

**a) Kigezo cha Maana**

Katika kigezo hiki, mofu huainishwa kwa kuzingatia maana inayowakilishwa na mofu inayohusika. Hii huwa maana ya kilekisika au ya kisarufi. Kwa kuzingatia kigezo hiki, tunapata mofu kuu tatu: mofu huru, mofu funge na mofu tata. Mofu hizi zinaweza kufafanuliwa kama ifuatavyo:

**i) Mofu Huru**

Mofu huru ni mofu ambayo hubeba maana ya kileksika iliyo kamilifu. Mofu hii huweza kukaa peke yake na kujisimamia kimaana. Mofu hii haihitaji msaada wa mofu nyingine ili iweze kueleweka. Naye Weber (1985), anasema kuwa mofu huru ni ile inayoweza kukaa peke yake kama neno kamili. Baadhi ya mizizi ya maneno huweza kukaa peke yake na kuwa na maana zinazojitosheleza. Mifano katika Na. (2a) – (2f) inaonesha mofu huru katika lugha ya Kiswahili:

(2) Mofu huru

a) Vivumishi:
{safi},{baridi}, na {hodari}

b) Viwakilishi:
{mimi}, {wewe}, {yeye}, {sisi}, {ninyi}, na {wao}

c) Nomino:
{baba}, {mama}, {Shangazi}, {Jembe}, na {soda}

d)Vihusishi:
{ndani}, {nje}, {Juu}, {chini}, {kando}, {Mbele}, na {nyuma}
e)Viunganishi:
{na}, {ila}, {au}, {ingawa}, na {ijapokuwa}
f)Vielezi:
{haraka}, {polepole}, {leo}, {upesi}, na {zamani}

Mifano Na. (2a) – (2f) inaonesha mofu huru ambazo zinaweza kukaa peke yake kama maneno kamili yenye maana kamili na inayoweza kueleweka bila kusaidiwa na mofu nyingine.

**ii) Mofu funge**

Mofu funge ni mofu tegemezi. Hii ni mofu ambayo haina uwezo wa kukaa peke yake kama neno kamili lenye maana inayojitosheleza. Mofu hii hutegemea mofu nyingine ili iweze kueleweka kimaana. Mifano katika Na. (3) – (5) inaonesha mofu funge katika maneno ya Kiswahili:

(3) a) Mtoto
**{m}** + {toto}
Kng1 + mz

b) watoto
**{wa}** + {toto}
Kng2 + mz

(4) a) Mti
**{m}** + {ti}
Kng3 + mz

b) miti
**{mi}** + {ti}
kng4 + mz

(5) a) Jitu
**{ji}** + {tu}
Kng5 + mz
b) majitu
**{ma}** + **{ji}** + {tu}
Kng 6 + kiambishi cha ukubwa + mz

Katika mifano Na. (3) – (5), tunaona kuwa kila neno limeundwa na mofu mbalimbali. Katika mifano hiyo, {m}, {wa}, {m}, {mi}, {ji}, {ma} na {ji} ni mifano ya mofu ambazo ni tegemezi. Mofu hizi huchangia maana za kisarufi za maneno hayo. Maana hizo ni kng 1, kng 2, kng 3, kng 4, kng 5, kng 6, na viambishi vya ukubwa wa nomino, mtawalia. Mofu za aina hii zikiondolewa katika mpangilio wa uundaji wa maneno hupoteza maana ya kisarufi inayochangiwa na mofu inayohusika.

**iii) Mofu tata**

Mofu tata ni zile ambazo hubeba maana zaidi ya moja. Mofu ya aina hii hudhihirika katika muktadha wa neno ambalo linatumika katika sentensi. Mfano Na. (6) unaonesha mofu tata katika neno la lugha ya Kiswahili:

(6) “Mama alimchezea mtoto.”
alimchezea
{a}+{li}+{m}+{chez}+{e}+{a}
Kk+knj+ky+mz+ktndea+kt

Katika mfano Na. (6), neno **alimchezea** lina utata. Neno hili lina mofu 6 ambazo ni: {a} + {li} +{ m} + {chez} + {e} + {a}. Kutokana na kuwapo kwa mofu {e}, neno hili lina maana zaidi ya moja. Kwanza, linamaanisha kuwa mama alimtumbuiza mtoto; pili, mama alimfanyia mzaha au utani. Mofu tata inayosababisha kuwapo kwa utata huu ni {e}.

**(b) Kigezo cha Maumbo au Mofolojia**

Kwa kuzingatia kigezo hiki, uainishaji wa mofu huzingatia umbo la mofu. Hivyo, kwa kutumia kigezo hiki, kuna aina kuu mbili za mofu ambazo ni mofu changamano na mofu kapa.

**(i) Mofu Changamano**

Mgullu (1999) anasema kuwa mofu changamano ni mofu ambazo huundwa kwa kuweka pamoja mashina au mizizi miwili ya maneno ambayo, katika mazingira mengine, yanaweza kutenganishwa na kila moja likawa neno kamili. Kwa mfano, mofu ‘mwanamaji’ na ‘mwanamwari’ kama inavyoonekana katika mfano Na. (7) hapa chini.

(7) a) Mwanamaji
Mwana + maji
b) Mwanamwali

Mwana + mwali

Tukichunguza maneno {mwanamaji na mwanamwali}, tunaona kwamba maneno haya yana mofu kadhaa kama ifuatavyo:
{mw}+ {ana} + {maji}
{mw} + {ana} + {mwari}

Kwa mtazamo wa muundo wa maneno haya, ni wazi kuwa yameundwa kwa mofu funge moja na mofu huru mbili. Hali hii inayafanya maneno haya kuwa changamano. Kwa hiyo, ni wazi kuwa mofu hii huundwa kwa kuweka pamoja mizizi miwili au zaidi ili kuunda neno moja.

**(ii) Mofu kapa**
Mofu kapa ni umbo lisilo dhahiri. Mofu hii huwa haina umbo la kifonolojia wala kiothografia. Maana ya mofu hii hujitokeza akilini mwa mzungumzaji. Mfano Na. (8a) – (8c) inaonesha mofu kapa katika lugha ya Kiswahili.

| | | |
|---|---|---|
| (8) | a) Sikio | masikio |
| | b) Tunda | matunda |
| | c) Sanduku | masanduku |

Maneno katika mfano Na. (8a) – (8c) yapo katika ngeli ya tano na sita. Maneno haya yameundwa na mofu kapa ambayo haiwezi kudhihirika kwa maandishi wala kutamkwa. Mofu hiyo kapa imewakilishwa na alama {Ø} kama inavyoonekana katika ufafanuzi ufuatao:

| | | |
|---|---|---|
| a) | {Ø} + {sikio} | {ma} + {sikio} |
| b) | {Ø} + {tunda} | {ma} + {tunda} |
| c) | {Ø} + {sanduku} | {ma} + {sanduku} |

Katika mifano Na. (8a) – (8c) tunaona kwamba mofu za kuonesha umoja hazionekani katika maneno {sikio, tunda na sanduku} lakini zinaeleweka na ziko ~~katika~~ akilini mwa watumizi wa maneno haya. Wanaisimu hutumia alama {Ø} kuonesha kuwa kuna mofu kapa ya umoja au wingi yanayotumika kuashiria maana kamili.

**Mofimu**
Mofimu ni kipashio kimojawapo cha kimsingi katika taaluma ya uundaji wa maneno. *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* (1990) inafasili mofimu kama kipashio kidogo amilifu katika maumbo ya maneno. Fasili hii inaonesha mofimu kama kipashio kidogo na, kwa sababu hiyo, umbo lake katika neno haliwezi kugawanywa zaidi katika vipashio vingine vidogo vyenye maana. Pili, mofimu ni kipashio

amilifu kutokana na kuwa kinawakilisha utendaji au kazi fulani katika neno. Kwa mujibu wa fasili hii, tunaona mofimu kama vipashio vidogo vyenye utendaji wa kisarufi wa lugha na, ambavyo, vikigawanywa zaidi vinaathiri maana na umbo la neno.

Wesama (2003) naye anaifasili mofimu kama kiambajengo cha neno chenye maana au kazi fulani na ambacho hakigawiki zaidi katika viambajengo vingine vyenye maana. Wesama anaitazama mofimu kuwa maana inayowakilishwa na kiambishi. Kiambishi hiki huambikwa kwenye neno kuwakilisha maana ya kisarufi na kilekisika. Mdee, Njogu na Shafi (2011) wanafasili mofimu kama kipashio cha lugha ambacho ni kidogo kuliko neno chenye maana ya kisarufi ambacho huungana na vipashio vingine kuunda neno. Kwa mujibu wa fasili hii, ni wazi kuwa Mdee na wenzake wanakubaliana na wanaisimu wengine kuhusu mtazamo kuwa mofimu ni maana au dhana inayowakilishwa na mofu. Pili, ni kipashio shirikishi kati ya vipashio vingine vya uundaji wa maneno. Mgullu (1999) anafasili mofimu kama dhana ya kidhahania ambayo ni maana inayowakilishwa au kusetiriwa katika mofu. Kulingana na fasili hii, Mgullu anaiona mofimu katika kiwango cha maana inayojitokeza katika viambajengo vya maneno.

Kwa kuzingatia fasili hizo zote, tunapata kuwa mofimu ni kipashio kidogo kabisa chenye maana dhahania chenye utendaji wa kisarufi katika maumbo ya maneno (maana au dhana inayowakilishwa na mofu). Maana dhahania hubebwa na kusetiriwa na vipashio vidogo ambavyo ni mofu katika neno. Maana inayojitokeza katika mofimu huwa ni maana ya kilekisika na kisarufi.

**Ubainishaji wa mofimu**

Mofimu, kama viambajengo vya maneno katika lugha, hujitokeza kwa namna mbalimbali. Maneno ya lugha yeyote huundwa kwa kiambajengo kimoja au zaidi. Ubainishaji wa mofimu katika Kiswahili huzingatia muundo wa kila neno, uorodheshaji wa viambajengo vya maneno, kutambua mizizi au viambajengo katika neno ambavyo haviwezi kubadilika (kimaumbo na kimaana), pamoja na kutambua ikiwa viambajengo vilivyogawanywa haviwezi kugawika zaidi na kupata maana inayowakilishwa na kila kiambajengo.

Maneno huundwa kwa viambishi na mizizi au mzizi peke yake. Kwa kuzingatia hatua za ubainishaji wa mofimu kimuundo, tunapata mofimu kuu mbili. Mofimu hizi ni mofimu huru na mofimu tegemezi.

**a) Mofimu Tegemezi**

Mofimu tegemezi ni vipashio au viambajengo vya maneno ambavyo haviwezi kusimama peke yake kuwakilisha maana ya kilekisika na kisarufi. Mara nyingi, mofimu ya aina hii huwa viambishi au mizizi. Hii ni kwa kuwa mizizi mingi hutegemea viambishi ili kuunda neno, na viambishi navyo ni lazima vipachikwe kwenye mizizi ya maneno ili kupata maana. Mifano Na. (9a) – (9b) inaonesha mofimu tegemezi katika lugha ya Kiswahili.

(9)

a) {**m} + {**toto}
b) {chez} +{**e} + {a}**

Kwa kuzingatia muundo wa maneno haya mawili, herufi zilizokolezwa **{m}, {a}** na **{e}** ni mofimu tegemezi. Hii ni kwa sababu zinategemea muktadha wa mofimu zingine ili kupata maana amilifu.

**(b) Mofimu Huru**

Kwa kuwa baadhi ya mizizi huweza kusimama peke yake kama maneno yenye maana, basi hapa ndipo tunapopata mofimu huru. Hivi ni vipashio ambavyo vina uwezo wa kusimama peke yake kama maneno yenye maana. Mifano Na. (10a) – (10d) inaonesha mofimu huru katika lugha ya Kiswahili.

(10)

a) {baba}
b) {sufuria}
c) {jembe}
d) {hodari}

Mofimu hizi ni maumbo kamilifu yenye maana ya kileksika na kisarufi. Mofimu hizi zina maana inayojisimamia na ambayo haitegemei muktadha wa viambajengo vingine. Maneno haya yakigawanyika katika vipande zaidi maana halisi huathirika.

Kwa muhtasari, mofimu ni kipashio kidogo cha neno chenye maana ya kisarufi na kileksika. Hiki ni kipashio ambacho hakiwezi kugawanyika zaidi na kubakisha maana. Mofimu huweza kuwa mzizi au kiambishi. Kuna aina mbili kuu za mofimu kutegemea umbo na maana. Mofimu huru na mofimu tegemezi. Mofimu huru ni aina ya mofimu ambayo inaweza kutokea peke yake kama umbo lenye maana ya kisarufi na kileksika. Mofimu huru ni maneno kamili kama vile nomino, vivumishi, viunganishi, viwakilishi na vitenzi mbalimbali.

**Dhana ya alomofu**

Alomofu ni dhana nyingine ya msingi ya kimofolojia. Dhana hii imepata fasili na wanaisimu mbalimbali. Wesana (2003), kwa mfano, anafasili alomofu kama maumbo tofauti yanayowakilisha mofimu moja yakiwa na maana ya mofimu hiyo hiyo. Kulingana na fasili hii, Wesama anaiona alomofu kama maumbo mbalimbali yanayowakilisha maana ya mofimu moja na ambayo hutokea katika mazingira tofauti kuwakilisha maana ya kisarufi au kilekisika. Kwa mfano, katika Kiswahili, kuna ngeli mbalimbali ambazo huwakilisha umoja na wingi wa mofimu (nomino) kama vile /m-~ki-~Ø~ji~/. Haya ni maumbo mbalimbali yanayowakilisha maana ya mofimu moja ya upatanishi wa kisarufi umoja. Tazama mfano Na. 11:

(11)

| | | | |
|---|---|---|---|
| a) | Mtoto | mlevi | mtu |
| b) | kisu | kioo | kitanda |
| c) | tunda | chungwa | yai |

Mifano ya (11a) –(11c) inaonesha maumbo mbalimbali yanayowakilisha maana ya mofimu moja ya upatanishi wa kisarufi ya umoja. Maumbo haya ni alomofu ya ngeli ya /M-/, ngeli ya /Ki-/ na ngeli ya /Ji/. Alomofu ya aina hii ni alomofu ya upatanishi wa kisarufi ya umoja (alomofu ya Umoja). Haya ni maumbo mbalimbali yanayowakilisha maana ya mofimu moja ya upatanishi wa kisarufi umoja.

Mgullu (1999) anafasili alomofu kuwa maumbo kadhaa yanayowakilisha mofimu moja katika mazingira maalumu yakiwa na maana ya kilekisika na kisarufi. Kwa mujibu wa fasili hii, ni wazi kuwa alomofu ni maumbo kadhaa yanayowakilisha mofimu moja. Tofauti anayoileta Mgullu katika fasili yake ni ubainishaji wa utokeaji wa alomofu ambayo haijaelezwa na wanaisimu wengine katika fasili zao. Hii ina maana kwamba alomofu kadhaa huweza kutokea katika mazingira tofauti yakiwa yanawakilisha maana ya mofimu moja. Kwa mfano, /wa-~mi-~vi-~ma-~Ø~} ni maumbo tofauti ambayo yanawakilisha maana ya kisarufi ya mofimu ya nomino kwa wingi. Tazama mfano wa nomino husika:

(12)

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| a) | ***wa***tu | walimu | wasichana | alomofu /wa/ |
| b) | ***mi***ti | mikeka | misumari | alomofu /mi/ |
| c) | ***vi***tanda | visu | vioo | alomofu /vi/ |
| d) | ***ma***tunda | maembe | mayai | alomofu /ma/ |
| e) | /Ø/nyumba | nyundo | televisheni | alomofu /Ø/ |

Mifano ya (12a) – (12 e) ~~ya~~inaonesha maumbo ya alomofu zinazobeba maana ya kileksika na kisarufi.

Kwa kuzingatia fasili hizi zote, tunaweza kusema kuwa alomofu ni kipashio chenye maumbo kadhaa. Pili, maumbo haya huwakilisha maana fulani inayojitokeza katika mofimu moja. Maana hii inaweza kuwa maana ya kisarufi au ya kilekisika. Na, mwisho, alomofu hutokea katika mazingira tofauti. Kwa hiyo, tunaweza kuhitimisha kwa kusema kuwa alomofu ni maumbo kadhaa yanayojitokeza katika mazingira maalumu yakiwakilisha mofimu moja ya kilekisika (neno) au kisarufi (matumizi).

**Ubainishaji wa alomofu**

Ubainishaji wa alomofu ni hali ya kutambua alomofu kama inavyojitokeza katika mofimu. Alomofu hubainishwa kwa kuzingatia muundo na maana ya vipashio vinavyounda mofimu au neno. Ubainishaji huu huchunguza maumbo na maana iliyosetiriwa katika maumbo husika. Kwa hiyo, hatua ya kwanza ni kubainisha mofimu katika neno. Mfano wa (13a) – (13d) inaonesha ubainishaji wa alomofu katika mofimu:

(13)

a) {**m} + {toto}**
b) **{m} + {tu}**
c) **{mw} + {iz} + {i}**
d) **{ki} + {tab} + {u}**

Katika ubainishaji huu, kila neno lina mofimu yake ambayo ni ama mzizi au kiambishi. Kiambishi kinaweza kuwa kimoja au zaidi. Kama katika nomino {**mwizi**}, tunaona kuwa maumbo yamegawanyika katika vipashio ambavyo ni mofimu na haviwezi kugawika tena kwani vikigawanywa huenda vikakosa maana.

Hatua ya pili ya ubainishaji wa alomofu ni kuorodhesha maumbo tofauti yaliyogawanyika. Uorodheshaji huo huzingatia maana inayoweza kuwa ya kilekisika au ya kisarufi. Mifano ya (14a) – (14c) inaonesha ubainishaji wa alomofu katika maneno ya mtoto, mwizi na kitabu.

(14)

a) {**m} + {toto}**
b) **{mw} + {iz} + {i}**
c) **{ki} + {tab} + {u}**

Mifano hii inaonesha alomofu {**m-}** katika nomino mtoto, {**Mw-**} katika nomino mwizi na **{Ki-}** katika nomino kitabu. Maumbo haya ni ya kisarufi, yanatumika kuwakilisha idadi ya umoja na wingi. Ubainishaji huu humsaidia mwanaisimu kutambua umbo msingi la maneno. Umbo msingi ni maumbo mbadala ambayo yanatumika kueleza maumbo mengine tofauti yenye maana sawa. Vilevile, kutokana na ubainishaji huu tunaweza kupata umbo kapa. Umbo kapa ni umbo ambalo halijitokezi kifonolojia wala kiothografia bali hutambulika kimaana katika akili za mzungumzaji wa lugha.

Alomofu hutokea katika mazingira maalumu. Mazingira ya alomofu ni kanuni au masharti ambayo ni lazima yazingatiwe ili alomofu iweze kutokea. Kanuni hiyo ni ya uambatizi wa viambishi katika mizizi. Kanuni hii ya kuambatisha viambishi katika maneno humsaidia mwanaisimu kutambua nafasi ya utokeaji wa alomofu. Kwa mfano, alomofu {**m-**} katika maneno kama {Mtu, msichana, mti na mkeka} huambatishwa katika mizizi ya maneno yanayoanza na konsonanti. Alomofu {**Mw**} huambatishwa katika mizizi ya maneno yanayoanza na vokali.

Kwa muhtasari, tunaweza kusema kuwa alomofu ni umbo linalowakilisha mofimu moja katika mazingira fulani likiwa limebeba maana ambayo ni ya kilekisika au kisarufi. Maumbo haya yanaweza kuwa maumbo ya kimsingi au maumbo kapa. Maumbo fulani yataitwa alomofu ikiwa yanabeba maana moja hata kama yanatokea katika mazingira tofauti. Ubainishaji wa alomofu huzingatia umbo msingi la alomofu na maana inayosetiriwa katika umbo msingi.

**Changamoto za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Mofolojia**

Changamoto ambazo zilijitokeza miongoni mwa wanafunzi kupitia mijadala shirikishi na usaili wa wanafunzi na walimu ni kuwa, istilahi zinazotumika katika kueleza dhana muhimu za kimofolojia ni ngumu na zinazokanganya sana. Wanafunzi walieleza kuwa usayansi wa istilahi za kimofolojia uliwawia vigumu kwao kueleza, kubaini, kuainisha na kuchambua dhana za kimofolojia kama vile mzizi na shina, muundo wa ndani na nje wa maneno, vipashio vya uundaji wa maneno, sarufi, mofu na mofimu, maumbo ya mofimu, mofimu yenyewe, maana ya kileksika na kisarufi hadi walipofafanuliwa kwa lugha ya kawaida.

Aidha, matumizi ya dhana mbili katika kueleza dhana moja ya kimofolojia ni tatizo kuu. Kwa mfano, kusema kuwa alomofu ni maumbo tofauti yanayowakilisha mofimu moja yakiwa na maana ya mofimu hiyohiyo. Dhana hii imepata istilahi mbili, mofu na mofimu. Istilahi hizi lazima zipate fasili yake kabla ya mwanafunzi kutambua maana ya alomofu.

Changamoto nyingine iliyotambulika ni ya uteuzi na uchache wa vitabu vinavyotumia lugha rahisi kuendana na umilisi wa wanafunzi husika. Aidha, vitabu vilivyoandikwa haviakisi umilisi na kiwango cha wanafunzi kwa sababu ya uchangamano wa lugha. Kwa mujibu wa wanafunzi, vitabu hivi vimeandikwa kwa ajili ya wanafunzi wenye umilisi wa kiwango cha juu kutokana na usayansi wa istilahi zilizotumika. Pia, ilifahamika kuwa baadhi ya vitabu vilivyoteuliwa na wahadhiri kwa ajili ya kutumika vilikuwa vigumu kwa wahadhiri na wanafunzi, hivyo kukwamisha ufundishaji na ujifunzaji wa mofolojia.

Utafiti vilevile uligundua kuwa kiwango cha umilisi, ufasaha wa lugha na maarifa ya kiwango cha chini cha baadhi ya wahadhiri na wanafunzi vilikwamisha ufundishaji na ujifunzaji wa mofolojia. Wahadhiri waliokuwa na umilisi, ufasaha na maarifa ya kiwango cha chini waliathiri mchakato wa ujifunzaji, kwani walishindwa kueleza dhana kwa ufasaha ili kuwaelewesha wanafunzi.

Aidha, umilisi wa kiwango cha chini wanafunzi nao ulikuwa kikwazo katika uelewa wa dhana za kimofolojia kwa sababu ya kutoelewa dhana husika zinapofundishwa na wahadhiri wenye weledi wa isimu. Wanafunzi wengi walishindwa kutunga sentensi kamili, kujieleza na kueleza dhana za mofolojia kutokana na umilisi mdogo waliopata kutoka madarasa ya juu. Waliojieleza vyema walikuwa na msingi wa ujifunzaji katika madarasa ya chini. Isitoshe, wanafunzi walikuwa na msimamo hasi kuwa mofolojia kama tawi la isimu ni ngumu kwa sababu ya kuzingatia kanuni na matumizi ya istilahi ngumu kueleza dhana za kawaida. Kwa ujumla, utafiti huu uligundua changamoto za kiisimu na zisizo za kiisimu zilivyoathiri ufundishaji na ujifunzaji wa mofolojia miongoni mwa wanafunzi kama ilivyoelezwa awali.

**Matokeo**

Utafiti huu ulibaini kuwa ufundishaji na ujifunzaji wa mofolojia pamoja na umilisi wa kiwango cha chini miongoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu nchini Uganda ulitokana na ugumu wa istilahi zinazotumika katika kueleza dhana muhimu za kimofolojia. Mijadala shirikishi na usaili uliofanywa ulidhihirisha ugumu wa wanafunzi kubainisha na kueleza dhana muhimu za mofolojia kama vile mzizi na shina, muundo wa ndani na nje wa maneno, vipashio vya uundaji wa maneno, sarufi, mofu na mofimu, maumbo ya mofimu (alomofu), pamoja na maana ya kileksika na kisarufi.

Aidha, ilibainika kuwa matumizi ya dhana mbili katika kueleza dhana moja yalikwamisha ujifunzaji na ufundishaji wa maarifa ya mofolojia. Mfano uliotolewa na wanafunzi ni ule wa fasili ya alomofu ambayo ilifasiliwa kuwa maumbo tofauti yanayowakilisha mofimu moja yakiwa na maana ya mofimu hiyohiyo. Fasili hii

iliwatatiza wanafunzi kwa kuwa dhana mbili za kisayansi (alomofu na mofimu) zilitumika kueleza dhana moja ya alomofu ambayo ilitarajiwa kuelezwa kwa lugha ya kawaida ili kueleweka vyema.

Vilevile, usaili wa wanafunzi na walimu ulidhihirisha kuwa baadhi ya wahadhiri waliofundisha mofolojia walikuwa na umilisi na maarifa ya kiwango cha chini cha ufundishaji wa isimu na hata ufasaha wa kujieleza na kueleza dhana muhimu za mofolojia kama ilivyo na wanafunzi walioonesha kuwa na umilisi wa chini wa matumizi ya Kiswahili sanifu. Viwango hivi vya umilisi na uzoefu wa kutumia Kiswahili baina ya mhadhiri na mwanafunzi ulikwamisha uelewa wa mofolojia miongoni mwa wanafunzi. Wahadhiri walidhihirisha kuwa wanafunzi wengi wana umilisi wa kiwango cha chini cha Kiswahili, hivyo mhadhiri wakati mwingine hulazimika kutumia lugha ya mazingira au Kiingereza katika kueleza dhana za mofolojia zilizo katika lugha ya Kiswahili. Katika kutumia mkakati huu, wanafunzi huzidi kutatizika kwa sababu ya usayansi wa istilahi za kiisimu.

Wanafunzi wanadai pia kuwa uchache na uteuzi wa vitabu mwafaka vya ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya isimu ulichangia kwa kiasi kikubwa kukwamisha ufundishaji na ujifunzaji wa mofolojia, ambapo wahadhiri walitumia vitabu vigumu katika kufundishia mofolojia ya Kiswahili. Ilibainika kuwa vitabu vingi viliandikwa na kuchapishwa Kenya au Tanzania, ambapo vingi vimeandikwa kwa lugha changamano (kisayansi). Vitabu hivi huakisi wanafunzi wenye msingi imara katika umilisi na ufasaha wa matumizi ya Kiswahili, aghalabu huwa wale wanaosomea shahada za umahiri na uzamivu. Hivyo, huwa haviendani na kiwango cha umilisi cha wanaoanza kujifunza Kiswahili wakiwa katika shule za upili.

**Mapendekezo**

Makala hii inapendekeza yafuatayo: Mosi, kuwe na utaratibu maalumu wa ujifunzaji na ufundishaji wa kozi za isimu kwa kutumia istilahi sahili. Pili, kuwe na usawazishaji wa istilahi na wanaisimu wanaoandika vitabu ili kuwasaidia wanafunzi kupata umilisi bora. Tatu, inapendekezwa vyuo vikuu kuandaa makongamano ya wanafunzi ili kuwasaidia wanafunzi kuimarika zaidi katika isimu. Nne, wataalamu wa isimu wanashauriwa kuandika vitabu kwa lugha sahili na vinavyoweza kusomwa na kutumika na wanafunzi wa viwango vyote vya umilisi. Tano, wahadhiri wanashauriwa kuwasaidia wanafunzi katika kuteua vitabu mwafaka na kuweka utaratibu wa kujadili dhana muhimu kwa kutumia lugha sahili ili kuwaelewesha vikamilifu na kuwahimiza wanafunzi kutumia Kiswahili katika shughuli zao. Sita, Kiswahili kipewe kipaumbele na kufundishwa katika shule za msingi kama somo la lazima ili kukuza umilisi, maarifa na ufasaha wa matumizi ya Kiswahili vyuoni.

**Hitimisho**

Makala hii imejadili mengi kuhusiana na dhana za kimsingi katika tawi la isimu la mofolojia na kuifafanua kwa lugha sahili ambayo inaweza kuchangia uelewaji wa dhana hizi muhimu. Ni wazi kuwa bila kuelewa dhana hizi inakuwa vigumu sana kwa msomi kuwa na umilisi wa kutosha wa taaluma hii ya mofolojia. Tukianzia kwa fasili, tumefafanua kuwa mofolojia ya Kiswahili ni taaluma ya isimu inayoshughulika na uchunguzi, uchambuzi wa maumbo ya maneno na aina za maneno katika Kiswahili. Vipashio vinavyochunguzwa ni mofu, mofimu, na alomofu.

Baada ya kuainisha na kubainisha dhana za kimsingi katika tawi la isimu la mofolojia, makala imebainisha changamoto za ufundishaji na ujifunzaji wa mofolojia zilizosababisha umilisi wa kiwango cha chini kwa wanafunzi wa vyuo vikuu nchini Uganda. Changamoto hizo ni kama vile usayansi wa istilahi, matumizi ya istilahi mbili kueleza dhana moja, misimamo hasi, umilisi na maarifa ya kiwango cha chini katika matumizi ya Kiswahili, pamoja na uchache na ugumu wa vitabu vinavyoteuliwa kutumika vyuoni. Kufuatia changamoto hizo, makala imependekeza mikakati ya ukuzaji wa taaluma ya mofolojia. Nayo ni: uandishi wa vitabu vya isimu vinavyoakisi umilisi wa wanafunzi, matumizi ya lugha sahili isiyo ya kisayansi kueleza dhana za kisayansi za mofolojia, ushiriki wa makongamano na warsha kwa walimu na wanafunzi, pamoja na kuteua vitabu mwafaka vya kufundishia isimu kutegemea umilisi wa wanafunzi na kadhalika.

**Marejeleo**

Abdalla, S.A (2016). Changamoto za Kutumia Istilahi Mbili kwa Dhana Moja Katika Kufundisha Isimu na Fasihi Shule za Sekondari: Mfano Kutoka Mkoa wa Kusini Pemba, Tanzania. Tasnifu ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (haijachapishwa).

Bakari, M. (1985). *The morphophonology of the Kenyan Swahili dialects*. Berlin Dietrich: Reimer.

Besha, R.M. (2007). *Utangulizi wa Lugha na Isimu*. Dar es Salaam: Macmillan Aidan Ltd.

Buliba, L. (1998). 'Utata katika Istilahi za Isimu ya Kiswahili.' Makala iliyowasilishwa katika kongamano la Kiswahili, Chuo Kikuu cha Kenyatta, 23-25 Septemba 1998.

Crystal, D. (2002). *The English language: A guided tour of the language*. London: Penguin.

Habwe, J.H. na Karanja, P. (2004). *Misingi ya sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix publishers Ltd.

Habwe, J.H. na Karanja, P. (2007). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili, Fonolojia, Mofolojia, Sintaksia na Semantiki*. Nairobi: Phoniex Publishers Ltd.

Hartmann, R.R.K. na Stork, F.C. (1972). *Dictionary of language and linguistics*. London: Applied Science Publisher.

Jaika, P. (2017). *Uchanganuzi wa Umilisi wa Kiisimu wa Wanafunzi wa Lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Maseno Nchini Kenya*. Tansifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Maseno

Kapinga, M.C. (1983). *Sarufi maumbo ya Kiswahili sanifu*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kihore, Y.M., Massamba, D.P.B. & Msanjila, Y.P. (2003). *Sarufi maumbo ya Kiswahili sanifu (SAMAKISA): sekondari na vyuo*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Marealle, I.B. (1978). "Dhana za Mofu, Mofimu na Alomofu." Katika: *Mulika Na. 13*. Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D.P.B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Massamba, D.P.B. (2009). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Mazrui, A.A. na Mazrui, A.M. (1995). *Swahili State and Society: The Solitical Sconomy of an African Language*. Nairobi: East African Publishers.

Massamba, D.P.B. Kihore, Y.M. na Hokororo, J.I. (1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA): Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D.P.B. (2010). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Mdee, J.S. (1999). *Sarufi ya Kiswahili: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: DUP.

Mdee, J., Njogu, K. na Shafi, A. (2011). *Kamusi ya Karne ya 21*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mgullu, R.S. (1999). *Mtalaa wa isimu: fonetiki, fonolojia na mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mgullu, R.S. (2009). *Mtalaa wa isimu: fonetiki, fonolojia na mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mgullu, R. (2018). 'Uhakiki wa Nakala ya Dhana za Mofu, Mofimu na Alomofu'. *Mulika Journal*, *20*(1).

Mlacha, S.A.K. (1995). *Kiswahili katika kanda ya Afrika Mashariki*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mukuthuria, M. (2006). Kiswahili and its expanding roles of development in East African cooperation: a case of Uganda. *Nordic Journal of African Studies, 15*(2).

National Curriculum Developmnet Centre (2018). Lower Secondary Curricculum Kiswahili Syllabus. National Curriculum Development Centre. Kampala, Kyambogo, Uganda.

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Wainaina, P., Buliba, A. na Gwachi, M. (2017). Athari za Uhawilishaji wa Miundo ya Kimofolojia kutoka Gĩkũyũ Hadi Kiswahili. *Mara Research Journal of Kiswahili-ISSN 2520-0577*, *2*(1), 60-73.

Weber, H. (1985). *A Dictionary of Phonetics and Linguistics*. London: Heinemann Educational Books.

Wesana-Chomi, E. (2003). "Sarufi Maumbo ya Kiswahili." African Studies Research Centre, *University of Sebha, Sebha, Libya*.
Wesana-Chomi, E. (2003). Kozi Fupi Tangulizi katika Sarufi Maumbo ya Kiswahili. African Studies Research Centre, *University of Sebha, Sebha*.

**VUFUPISHO:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| {Ø} | Alama dhahania | Kng | Kiambishi ngeli |
| mz | Mzizi wa neno | KK | Kiambishi kiwakilishi |
| knj | Kiambishi cha njeo | Kt | Kiambishi tata |
| L1 | Lugha ya kwanza | L2 | Lugha ya pili |
| Na. | Namba | | |
| Ktndea | kiambishi nyambulishi cha kutendea | | |
| Kng 1, 2.... | Ngeli ya kwanza, pili, nakadhalika | | |
| NCDC | Nationala curriculum Development centre | | |